

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA TATU**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI**

**16 MEI, 2016**

## **MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI**

**TAREHE 16 MEI, 2016**

### **I. DUA**

Saa 3.00 asubuhi Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

#### **Makatibu Mezani**

1. Ndg. Ramadhani Abdallah
2. Ndg. Asia Minja

### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

1. Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
2. Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
3. Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
4. Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2016/2017.

### **III. MASWALI:**

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge;

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Swali Na.165 – Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni (kny. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga)

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Raphael Masunga Chegeni

(ii) Mhe. Mary Pius Chatanda

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na.166 – Mhe. Lucy Michael Mlowe

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Lucy Michael Mlowe

(ii) Mhe. Hamidu Hassan Bobali

Swali Na.167 – Mhe. Kemilembe Julius Lwota [kny. Stanslaus Mabula]

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Kemilembe Julius Lwota

(ii) Mhe. Suzan Anselm Lyimo

(iii) Mhe. Abdallah Hamisi Ulega

Swali Na.168 – Mhe. Albert Ntabaliba Obama

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Albert Ntabaliba Obama

(ii) Mhe. Cecilia Daniel Paresso

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na.169 – Mhe. Prosper Joseph Mbena

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Prosper Joseph Mbena

(ii) Mhe. Anthony Calist Komu

(iii) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Swali Na.170 – Mhe. Oran Manase Njenza

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Oran Manase Njenza

(ii) Mhe. Shaban Omar Shekilindi

(iii) Mhe. Charles John Tizeba

(iv) Mhe. Hussein Nassor Amar

(v) Mhe. Janet Zebedayo Mbene

Swali Na.171 – Mhe. Moshi Selemani Kakoso

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Moshi Selemani Kakoso

(ii) Mhe. Ester Amos Bulaya

(iii) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

(iv) Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa

Swali Na.172 – Mhe. Godfrey William Mgimwa

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Godfrey William Mgimwa

(ii) Mhe. Jerome Dismas Bwanausi

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na.173 – Mhe. Saumu Hery Sakala [kny. Mhe. Mussa Bakar Mbarouk]

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Saumu Hery Sakala

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Swali Na.174 – Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Immaculate Sware Semesi

### **IV. MATANGAZO:**

1. Wageni wote waliokuwepo Bungeni walitambulishwa.
2. Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitangaziwa kuwa na Kikao saa Saba Mchana.
3. Wabunge wachezaji wa mchezo wa mpira wa wavu na kikapu walitangaziwa kujiandikisha chumba Na. 329.
4. Mhe. Godfrey William Mgimwa aliomba Naibu Waziri wa Nishati na Madini arekebishe taarifa yake kwani kwenye swali lake la nyongeza alisema ni Mbunge wa Morogoro yeye ni Mbunge wa Iringa. Mwenyekiti alisema Kanuni ya 45(3) itatumika.

### **Taarifa ya Spika:**

Mwenyekiti alielekeza Kamati ya Kanuni kukutana kupitia Taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kujiridhisha kama imekidhi matakwa ya Kanuni. Mhe. Godbless Lema na Mhe. Freeman Mbowe wahudhurie kikao hicho. Pia alieleza endapo muda wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuwasilisha maoni yake utafika na kama bado Kamati haijamaliza kazi yake ataelekeza nini cha kufanya.

### **Mwongozo wa Spika:**

1. Mhe. Kemilembe Julius Lwota alitumia Kanuni ya 68(7) kutaka kujua Serikali inatoa kauli gani kuhusu video ya udhalilishaji mwanamke inayosambaa kwenye mitandano. Waziri wa Afya alieleza Serikali inakemea vikali tukio hili na tayari wahusika wameshakamatwa na wakati wowote watafikishwa Mahakamani na alitoa rai kwa watu wote kuacha mara moja kusambaza tukio/video hiyo.
2. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa aliomba mwongozo kwamba Taarifa ya Upinzani ni ya Kambi nzima na siyo ya Mhe. Godbless Lema pekee na akaeleza inavyoonekana kama Kambi inataka kuambiwa nini cha kuandika na endapo taarifa yao ina upungufu Serikali wakati wa kujibu

hoja itaelezea. Mwenyekiti alisisitiza kwamba alichosema ni Kamati ya Kanuni ijiridhishe na hajasema waandae taarifa hiyo.

3. Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi aliomba mwongozo kwamba nini kifanyike kwa Naibu Waziri wa Afya kwa vile amelidanganya Bunge kwa kusema vituo vya Afya alivyoulizia Mhe. Susan Anselm Lyimo taratibu za makabidhiano hazijakamilika wakati ni miaka miwili majengo hayo yamekabidhiwa Serikalini. Kiti kiliahidi kutoa majibu baadae.
4. Mhe. John Wegesa Heche alitumia Kanuni ya 68(7) akiomba mwongozo kuhusu Polisi kuvamia kituo cha afya cha Sungusungu – Tarime na kuwapiga risasi Wananchi – Mwenyekiti aliahidi kulitolea maelezo jambo hilo baadaye.

#### **V. HOJA ZA SERIKALI:**

- Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.
- Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aliwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **VI. KUSITISHA BUNGE:**

Mhe. Jenista Mhagama alitoa Hoja kwa kutumia Kanuni ya 28(2) (3) Bunge lisitishwe Saa 11.44 ili Kamati ya Kanuni imalize kazi.

#### **VII. BUNGE KUREJEA:**

Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Mussa Azzan Zungu.

#### **Taarifa ya Spika:**

Taarifa ya Kamati ya Kanuni iliyopitia Taarifa ya ya Kambi Rasmi ya Upinzani kujiridhisha kama haijakiuka Kanuni. Kamati ya Kanuni iliagiza baadhi ya vipengele viondolewe. Kanuni ya 64(1) (c) (d) na (f) imekiukwa na imeamua yaondolewe.

Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alipoitwa kusoma taarifa yake, Mhe. Godbless Lema alisema kutokana na Mwongozo wa Kiti hana sababu ya kusoma maoni yao.

### **Uchangiaji wa jumla:**

Uchangiaji wa jumla uliendelea na wafuatao walichangia:-

1. Mhe. Dkt Shukuru Kawambwa	-	CCM
2. Mhe. Almas Athuman Maige	-	CCM
3. Mhe. Allan Joseph Kiula	-	CCM
4. Mhe. Masoud Abdallah Salum	-	CUF
5. Mhe. Yusuf Haji Khamis	-	CUF
6. Mhe. Esther Nicholas Matiko	-	CHADEMA
7. Mhe. Yusuf Kaiza Makame	-	CUF
8. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda	-	CCM
9. Mhe. Emmanuel Elibariki Kingu	-	CCM
10. Mhe. Godbless Jonathan Lema	-	CHADEMA
11. Mhe. Peter Joseph Serukamba	-	CCM

### **Taarifa:**

Mhe. Kabwe Ruyagwa Zitto alitoa taarifa kwa mzungumzaji kwamba Kamati ya PAC mwaka 2013 ndiyo iliagiza suala la Lugumi lichunguzwe hivyo mzungumzaji analipotosha Bunge. Aidha, alipotaja jina la Rais Wapinzani walisema hatakiwi kutajwa lakini Mwenyekiti alitoa mwongozo kwamba Rais hatakiwi kutajwa kwa kejeli.

12. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa	-	CHADEMA
----------------------------------	---	---------

Mwenyekiti alimtaka Msigwa kutozungumzia sakata la nyumba ambalo wa kiti kimeshalitolea mwongozo. Kiti kilitoa mwongozo wa pande zote mbili kuzingatia Kanuni kuzungumza bila kupata ruhusa ya kiti.

### **Kuhusu utaratibu:**

Mhe. Jenista Mhagama alitumia Kanuni ya 64 akisema Mhe. Msigwa ametumia maneno ya kuudhi kusema Serikali imetoa macho nk. na kuomba azingatie Kanuni. Kiti kiliagiza Mhe. Msigwa kumalizia kuchangia kwa kuzingatia Kanuni.

13. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola	-	CCM
14. Mhe. Mary Pius Chatanda	-	CCM
15. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare	-	CHADEMA
16. Mhe. Khatib Said Haji	-	CUF
17. Mhe. Alli Hassan Omar King	-	CCM

### **KUHITIMISHA HOJA:**

1. Mhe. Nape Moses Nnauye – Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo.
2. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. George Mcheche Masaju
3. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Hamad Yussuf Masauni
4. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi , Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga

### **VIII. KAMATI YA MATUMIZI**

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi na kupitia Vifungu vya Wizara. Waziri alita Taarifa ya kazi ya Kamati na kisha kutoa Hoja, Bunge lilihojiwa kuhusu Hoja hiyo na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Pia Wabunge wa Upinzani walitoka nje kutokana na hoja ya Mashehe waliyoitoa.

#### **Bunge lilirudia**

Waziri wa Mambo ya Ndani alitoa hoja na Bunge lilihojiwa na kuafiki.

#### **Mwongozo wa Spika**

Mhe. Kabwe Ruyagwa Zitto aliomba mwongozo kuhusu hoja za Mashehe ambayo ilisababisha baadhi ya Wabunge kususia Kikao cha Bunge siku hiyo kwamba Bunge lichunguze hoja hizo kwa kuunda Tume huru (*Independent Commission*) ya kupitia ripoti ya Madaktari kwani suala hili litagawa nchi. Kiti kiliahidi kutoa majibu baadaye.

### **IX. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Saa 2.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 17/5/2016 siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA  
16 MEI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**